# MEASLES

## Usiruhusu mtoto wako augue ugonjwa huo - wapewe chanjo ya MMR

- Ukambi umegonga vichwa vya habari tena. Kumekuwa na kuzuka kukali kwa ukambi huko Wales na Uingereza na idadi ya watoto wanaopata ugonjwa huu inaongezeka.
- Ukambi unaweza kuwa ugonjwa mkali sana, ambao unasababisha maambukizi ya sikio na kifua, kukohoa, kuhara na uharibifu wa ubongo. Ukambi unaweza kuua.
- Mtoto wako ako katika hatari ya kupata ugonjwa wa ukambi ikiwa hajapokea chanjo ya MMR.
- Vipimo viwili vya chanjo ya MMR vinahitajika ili kupata ulinzi bora zaidi.
- Ikiwa mtoto wako anafaa kupokea vipimo viwili vya chanjo ya MMR lakini bado hajapokea, bila kujali umri wake, unapaswa kuwasiliana na GP wako ili ampe chanjo haraka iwezekanavyo. *
- Ikiwa huwezi kukumbuka ikiwa mtoto wako amepata kipimo chochote cha chanjo moja au mbili za MMR, angalia rekodi yake ya afya ya kibinafsi (Kitabu Kikuu). Ikiwa kufanya hivi hakutasaidia, zungumza na GP wako.
- Ikiwa hujui ni kipimo kiasi gani alichonacho mtoto wako, ni bora kuwa na vipimo viwili vya chanjo ya MMR sasa hivi badala ya kumuhatarisha kwa kumuacha bila ya ulinzi.

*Ili kukabiliana na kuzuka kwake katika maeneo, basi vipimo viwili vinaweza kupeanwa vikiachana na mwezi mmoja baada ya umri wa miezi 18.

**immunisation**

njia salama zaidi ya kulinda mtoto wako

Maswali mengine ya kawaida kuhusu ukambi na chanjo ya MMR yameorodheshwa nyuma ya kipeperushi hiki

# Majibu ya baadhi ya maswali ya kawaida kuhusu ukambi na chanjo ya MMR

## Je, kwa nini tunaona kuzuka huku kwa ukambi?

Ukambi ni ugonjwa unaoambukiza sana, husambazwa haraka kutoka mtu mmoja hadi mwingine, hasa shuleni. Mtoto mwenye ukambi ataambukiza watoto karibu wote ambao anakaribiana nao. Tangu mwishoni mwa mwaka wa 2017 kumekuwa na ongezeko la ukambi duniani kote ambalo limeathiri Uingereza. Hii imesababisha kuenea katika jumuiya pana, hususan katika makundi yaliyo na kiasi kidogo cha chanjo.

## Je, chanjo za MMR mara nyingi hupeanwa wakati gani?

Nyakati bora ni kati ya umri wa miezi 12 na 13 na tena katika miaka mitatu na miezi minne, kwa kipimo kimoja kwa kila tukio. Lakini, ikiwa mtoto wako hakuwa amepata chanjo awali, anaweza kupewa chanjo katika umri wowote na vipimo viwili vinavyoachana na mwezi mmoja.

## Je, kuna madhara yoyote ya chanjo?

Mtoto wako anaweza kupata dalili za ukambi, matone na rubella kwa hadi wiki sita baada ya chanjo lakini kwa hali isiyo kali sana. Hii inathibitisha kwamba chanjo inafanya kazi na mtoto wako anajenga kinga ya siku zijazo za kupata virusi vinavyosababisha magonjwa haya matatu. Sio watoto wote wanaoonyesha dalili hizi lakini hiyo haimaanishi chanjo haifanyi kazi.

## Je, wazazi walio katika maeneo yaliyozuka ukambi wanapaswa kupewa chanjo dhidi ya ukambi?

Kama ilivyo na magonjwa mengi, mara tu unapokuwa na ukambi, huwezi kupata tena kwa sababu umejenga kinga asilia dhidi yake. Kwa hivyo, ikiwa ulikuwa na ukambi au vipimo viwili vya chanjo ya MMR huhitaji kupata chanjo sasa hivi.

---

Kwa maelezo zaidi kuhusu ukambi na MMR nenda kwenye
**www.nhs.uk/conditions/measles/**

© Crown copyright 2023. Product code: M23SWA. UKHSA Gateway Number 2023256. 1P 200k August 2023 (APS) – Schools version

This is a Swahili translation of the measles dont let your child catch it – English version. There are also versions in Afrikaans, Arabic, Bengali, Cantonese, simplified Chinese, French, German, Hebrew, Hindi, Italian, Lithuanian, Polish, Portuguese, Romani, Romanian, Spanish, Tagalog, Tamil, Turkish, Ukrainian and Urdu. If you would like more copies of this leaflet or any other immunisation publications please visit www.healthpublications.gov.uk or call 0300 123 1002

NHS
Maelezo ya Chanjo